
# Urithi WETU

11 WANYAKYUSA NA HISTORIA YAO YA KUPENDEZA
12 WIZARA NA MWELEKEO MPYA KATIKA SEKTA YA BIASHARA



# Usiyoyajua kuhusu hifadhi ya Gesimasowa

## * Ndege anayesafiri dunia nzima hupumzika hapa



Milima ya Livingstone iliyopo mwambao mwa Ziwa Nyasa eneo la Chiwindi ambapo pia ndege hupumzika kwa muda.

Na Albano Midelo

Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa nchini ambayo imebarikiwa kuwa na neema ya vivutio lukuki na adimu vya utalii wa ikolojia na kiutamaduni.

Hifadhi ya Gesimasowa yenye ukubwa wa kilometa za mraba zaidi ya 760 ambayo ipo katika Halmashauri ya Madaba, Wilaya ya Songea, ni miongoni mwa vivutio adimu vya utalii.

Hifadhi hiyo ilianzishwa kama msitu wa hifadhi mwaka1975 na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma wa zamani Dk Lawrence Gama mwaka 1975.

Hatimaye mwaka 2015, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma katika kipindi hicho hayati Said Mwambungu alisimamia mchakato wa kupandisha hadhi msitu huo na kuwa hifadhi ya Taifa.

Moja ya vivutio vilivyopo katika hifadhi hii ni mapumziko ya ndege maarufu duniani wanaozaliana katika Hifadhi ya Taifa ya Kitulo iliyopo Makete mkoani Njombe wanaoitwa kitaalam Derhams wenye uwezo wa kuruka toka bara moja hadi bara jingine.

Ofisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe anabainisha kuwa ndege hao wanapumzika hapa kwa miezi kadhaa kisha wanaendelea na safari kupitia bonde la ufa hadi Ziwa Nyasa hatimaye wanasafiri hadi nchini Afrika Kusini na mabara mengine.

Kulingana na Challe, Hifadhi ya Gesimasowa ni mapito ya ndege hao wanatoka Kaskazini mwa Afrika kuelekea Afrika ya Kusini ambao wanafuata milima ya Livingstone iliyopo Ziwa Nyasa.

Aidha inaelezwa kwamba ndege hao pia wanapumzika mwambao mwa Ziwa Nyasa hasa katika eneo la Kihagara ambapo kuna mazingira yanayovutia ndege hao kuishi na kuongeza uzuri wa tunu kubwa ya eneo hilo.

Kwa mujibu wa Challe, Hifadhi ya Gesimasowa pia ina mfumo wa ikolojia wa pori la Selous ambalo sasa ni Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa sababu ni mapitio

Inaendelea Uk. 13

Scanned with CamScanner

# ... hifadhi ya Gesimasowa

Inatoka Uk. 9

mapitio ya wanyamapori wanaotoka katika Pori la Akiba la Selous.

Wanyama hao ni wale wanaopita kuelekea Bonde la Ziwa Nyasa kupitia pori la Liparamba hadi Hifadhi ya Niasa nchini Msumbiji ambapo wanyama wanakwenda nchini Msumbiji na kurudi Tanzania.

"Kikao cha Ushauri cha Mkoa wa Ruvuma kimeridhia hifadhi hii kupandishwa hadi kuwa Pori la Akiba la Gesimasowa. Mchakato wa kutangaza rasmi katika Gazeti la Serikali kwamba Gesimasowa kuwa Pori la Akiba upo katika hatua za mwisho", anasisitiza Challe.

Wanyama ambao unaweza kuwaona katika hifadhi ya Gesimasowa ni tembo, simba, ndege, nyati, pofu na samaki adimu duniani aina ya mbelele na mbasa.

Hamasa kubwa inahitajika kuhakikisha kuwa wageni na wazawa wanajitokeza kwa wingi kutembelea hifadhi hii ili kujionea uzuri wake na kuitangaza zaidi.

Hifadhi hii pia ni maingiliano ya mito miwili ya Hanga na Lutukira ambayo inatengeneza mto Ruhuhu unaomwaga maji yake Ziwa Nyasa. Mto huo ndiyo mazalia ya samaki aina ya mbelele na mbasa ambao katika duniani nzima wanapatikana Ziwa Nyasa pekee.

"Samaki hawa ni adimu sana kwa sababu utafiti umebaini samaki hawa wanapatikana Ziwa Nyasa pekee na wanazaliana katika Mto Ruhuhu ambao unachangia asilimia 20 ya maji katika Ziwa Nyasa", anasema Challe.

Utafiti wa samaki aina mbasa na mbelele katika Mto Ruhuhu na Ziwa Nyasa ulifanywa na Fransis Challe mwaka 2010 ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) Kitivo cha Sayansi, Teknolojia na Mazingira na chapisho la utafiti huo lilitolewa mwaka 2011.

Hata hivyo Challe anasema wavuvi katika Ziwa Nyasa wanafanya uharibifu wa mazingira kwenye maingiliano ya Mto Ruhuhu na Ziwa Nyasa eneo la Folkland Lituhi ambapo wanaharibu vifaranga wa samaki hao ambao wanaingia katika Ziwa Nyasa.

Uchunguzi umebaini kuwa katika hifadhi ya Gesimasowa ambako samaki wanazaliana wananchi wamefanya uharibifu mkubwa wa mazingira kwa kukata miti ambayo ni muhimu katika chanzo hicho cha Mto Ruhuhu.

Challe anasisitiza eneo la maingiliano ya Mto Hanga na Mto Lutukira lililopo katika Hifadhi ya Gesimasowa linatakiwa kulindwa na kuhifadhiwa ili kuhakikisha hazina hiyo haipotei kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vya baadae.

"Samaki wanazaliana hapa kwenye maingilio ya mito, kisha wanasafiri hadi Ziwa Nyasa na kuendelea na maisha ambapo wakati wa kuzaliana samaki hao wanarudi tena hapa. Hivyo hili ni eneo muhimu sana kitaifa na kimataifa katika uhifadhi na utalii kwa kuwa samaki hao hawapatikani sehemu nyingine yoyote duniani", anasisitiza Challe.

Hata hivyo anasema Hifadhi ya Gesimasowa bado ni mpya na kwamba lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa maliasili zilizopo katika hifadhi hiyo zinalindwa ili ziwe endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Kulingana na Sheria ya Wanyamapori Namba 3 ya mwaka 2009, wananchi hawaruhusiwi kufanya shughuli zozote ndani ya hifadhi hizo. Wananchi wanajua kabisa hizi ni hifadhi kisheria, hivi sasa tunatekeleza maagizo ya Waziri Mkuu kuhakikisha kuwa wavamizi wote wa maeneo ya hifadhi tunawaondoa", anasema Challe.

Kwa mujibu Challe hivi sasa wanyamapori wanahama kutoka Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, wakipitia Hifadhi ya Gesimasowa, Litumbandyosi, Liparamba na kuvuka mpaka hadi Hifadhi ya Niassa nchini Msumbiji.


Akizungumzia hatua ambazo Idara ya Maliasili na Utalii inazichukua ili kuhakikisha hifadhi hizo zinalindwa, Challe anasema serikali imeanza kuchukua hatua ikiwemo kuweka alama kubwa za kudumu ili kutenganisha maeneo ya hifadhi na wananchi.

"Tumeanza kutoa elimu kwa wananchi wavue samaki kitaalam bila kuathiri mazalia ya samaki kwa kufuata nyavu zenye matundu yanayokubalika kisheria na kwamba endapo mazalia ya samaki yataharibiwa samaki hao wanaweza kutoweka duniani", anasisitiza Challe.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema ambaye Hifadhi ya Gesimasowa ipo katika wilaya yake anatoa rai kwa wananchi kuacha kukata miti kwenye kingo za mito na kuacha kuvua samaki kwa kutumia nyavu haramu kwenye maingiliano ya Mto Ruhuhu ili samaki aina ya mbasa na mbelele wasitoweke duniani.

Mgema anasema tayari wametekeleza agizo la serikali la kuweka mipaka kwenye hifadhi za misitu, mapori na kwenye mapito ya wanyamapori ili kuwadhibiti wananchi wanaovamia maeneo ya hifadhi na kufanya uharibifu mkubwa.

"Vijiji vingi vinavyopakana na hifadhi vinakuwa havijui mipaka yao, ndiyo maana serikali imeamua kufanya zoezi la kuweka alama za kudumu zinazoonekana kwenye maeneo yote ili kuondoa hisia za wananchi kuchukuliwa maeneo yao", anasema Mgema.



Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema alipotembelea Hifadhi ya Gesimasowa, hivi karibuni.

**Mwandishi ni Ofisa Habari Mkoa wa Ruvuma**
**Mawasiliano albano.**
**midelo@gmail.com,simu 0784765917**

TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

**MALIPO YA KODI KWA AWAMU NA UWASILISHAJI RITANI KWA WAKATI**

Ndugu Mlipakodi, unakumbushwa kulipa kodi ya mapato ya mwaka 2021 kadri ya awamu yako pamoja na kuwasilisha ritani ya kodi ya mapato ya mwaka 2020. Aidha, kama bado hujakadiriwa kodi ya mapato kwa mwaka 2021 tafadhali fika pia TRA ukadiriwe.

Wahi sasa ili kuepuka usumbufu usio wa lazima!.

TAHADHARI: Kuwa makini na matapeli wanaotumia vibaya jina la TRA au majina ya watumishi katika kipindi hiki, hivyo jiridhishe kila wakati.

*Kumbuka: Ukiuza toa risiti. Ukinunua dai risiti*

Kwa maelezoa zaidi, piga simu bure;
0800-750075 au 0800-780078
Barua pepe: huduma@tra.go.tz WhatsApp: 0744-233-333

SQ001775

Scanned with CamScanner